**Embassy of the Islamic Republic of Iran-Nairobi**

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU

# TAMASHA LA VIBONZO ULIMWENGUNI LA KUTUMIA SANAA NA UTAMADUNI KATIKA KUNYAMAZISHA SILAHA BARANI AFRIKA

**MRATIBU:** Ubalozi wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran nchini Kenya

Katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, juhudi nyingi zimefanywa kupambana na athari za bunduki barani Afrika, na hii ni hatua nzuri ya kufikia Afrika isiyo na mizozo. Licha ya juhudi hizi, mizozo imeendelea katika sehemu nyingi za bara la Afrika. Misimamo mikali, tishio la ugaidi na jinai za kimataifa katika bara hili bado ni changamoto inayoendelea.

Silaha, kama chombo maarufu zaidi barani, kimevutia maoni ya wanachama wa nchi zilizoko kwenye Umoja wa Afrika na kuzua mpango wao wa kukomesha matumizi mabaya ya silaha barani Afrika.Madhumuni kuu ya mpango huu ni kufanikisha Afrika isiyo na mizozo, kuzuia mauaji ya kimbari, kufanikisha amani kwa wote na kusafisha bara la Afrika kutokana na vita, mzozo mkali, ukiukwaji wa haki za binadamu na majanga ya kibinadamu.

Ili kuharakisha mpango huu, Umoja wa Afrika ulizindua mradi wa "Kunyamazisha Bunduki" mnamo 2020 kwa kuhamasisha wadau wote. Lakini janga la COVID-19 mnamo 2020 lilituzuia kushughulikia suala hili muhimu barani Afrika vizuri. Mada ya Umoja wa Afrika ya 2021 "Sanaa, Utamaduni na Urithi" ilituchochea kutumia sanaa kuweka hafla hii muhimu mwaka ujao na kujitahidi kuifanikisha.

Ubalozi wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran nchini Kenya, sambamba na juhudi za Umoja wa Afrika, wameamua kufanya tamasha la vibonzo Ulimwenguni la “Kunyamazisha Bunduki" likiwa juhudi makusudu linaloonyesha kuwa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, inaendeleza uhusiano wake na nchi za Afrika kwa kufanikisha amani na maendeleo katika bara.

**ANWANI:**
Tamasha la vibonzo Ulimwenguni juu ya unyamazishaji wa Silaha barani Afrika

**MADA NDOGO:**

1. Hatia kwa matuzima ya bunduki katika usuluhishaji wa mzozo
2. Unyamazishaji wa silaha na Mizizi ya migogoro (umasikini, ukosefu wa haki wa kihistoria na usawa, mabadiliko ya hali ya hewa, mizozo ya ukabila)
3. Biashara ya silaha na vita

4. Hukumu ya Mauaji ya Kimbari na uhalifu wa kivita
5. Kukabiliana na msimamo mkali na ugaidi
6. Unyamazishaji wa silaha na haki za kibinadamu
7. Kuzunguka kwa silaha na kupunguza migogoro ya vurugu
8. Athari za Kunyamazisha silaha kwa kizazi kijacho cha Kiafrika, kizazi cha amani na mazungumzo
9. Kutumia sanaa na utamaduni katika unyamazishaji wa silaha

**Siku ya mwisho ya kutuma kazi ya Sanaa:** Tarehe 1, Julai 2021 (kabla ya saa 12 usiku wa manane)

**Masharti:**

- kila mwana vibonzo anaruhusiwa kutuma kazi zake tano tu za Sanaa.
- kazi ya Sanaa iwe kwa kiwango Cha A4 na itumwe kwa njia ya JPEG  na azimio la 300DPI;
- Fomu za kujisajili lazima ziwe zimekamilika katika Kila kazi ya sanaaa;
- kazi yenyewe isiwe imetumika katika tamasha zozote na isiwe imechapishwa popote;
- mbinu zozote za kuimarisha kazi yako lazima zitumike;
- kazi zote za Sanaa zifuate sheria za uchapishaji;
- kwa kutuma kazi zote za Sanaa,Kila mwana vibonzo amehakikishiwa kuwa yeye ndiye mmiliki wa kazi hiyo na awape idhini wahakiki kuichapisha popote pale bila vikwazo.

**TUZO:**

UCHAGUZI WA WAAMUZI
Mshindi wa kwanza_dola 4,000 US
Mshindi wa pili dola 3,000 US
Mshindi wa tatu_dola 2,000 US

Sanaa tano zilizochaguliwa na majaji pia watapewa vyeti.

Mshindi wa kwanza wa Kenya atakaye chaguliwa na majaji: $400 + Cheti

Mshindi wa pili: $300 + Cheti

Mshindi wa tatu : $200 + Cheti

Tarehe ya kutangaza matokeo ya uteuzi: Julai 2021 kwa tovuti ya Ubalozi wa Irani: https://kenya.mfa.gov.ir/en na Facebook: @Iran.Kenya

Barua pepe ya kutuma kazi za sanaa: Silencefest2020@gmail.com

Kwa habari zaidi bonyeza: https://Kenya.mfa.gov.ir